

Taarifa za idadi za Jumuiya za watumia Maji zilizo udwa ndani ya Bonde la ziwa Victoria

Nivyombo vya kijamii vilivyo undwa na kusajiliwa chini ya Sheria Usimamizi wa Rasilimali za maji nchi 11 ya mwaka 2009 kifungu kidogo cha 81(1) Vinavyo shirikisha watumia maji wa aina mbalimbali katika bonde husika ili kusimamia kulinda na kugawa rasilimali za maji katika usawa. Jumuiya za watumia maji zinahusika na uhifadhi wa vyanzo vya maji, kutatua migogoro ya maji, na kusimamia shughuli za kiuchumi kama vile umwagiliaji.

Bodi ya Maji Bonde la ziwa Victoria lina jumla ya madakio ya maji matano ambayo kwakila dakio Bodi imefanikiwa kuunda jumuiya za watumia maji. Bodi imefanikiwa kuunda jumla ya vyanzo vya watumia maji (Jumuiya za watumia maji) 30 katika madakio yote.

Dakio la Kagera Jumuiya ya watumia maji Mtongono, RWAMILINGA, Kamirabingo, Kaburuma, Mwisu na Rwakajunju zikiwa dakio la Kagera.

Dakio la Isanga kuna Jumuiya za watumia maji Nyankanga, Ligembe juu, Ligembe chini na Jumuiya yawatumia maji Ihelele.

Dakio la Magogomuame lina jumuiya moja ambayo ni Jumuiya ya watumia maji Mto Mirongo.

Dakio la Simiyu lina jumla ya jumuiya za watumia maji 9 ambazo ni Jumuiya za watumia maji Sangijo, Minzimilu, Zanzui, Itunda, Nyamadunga, Malya, Simiyu kati, Lamadi na Jumuiya ya watumia Maji Nasa.

Dakio la Mara lina jumuiya za watumia maji 11 ambazo ni Jumuiya ya watumia maji Tigite juu, Tigite chini, Tobora Juu, Tobora chini, Eneo Oevu Mto Mara Kaskazin, Mara kusi, Somoche juu, Somoche Chini, NYASULUGI na Jumuiya ya watumia maji Manchira